# JINSI YA KUZALISHA AZOLLA KAMA CHAKULA CHA KUKU





Azolla ni aina ya blue green algae ambayo huweza kulimwa na kustawi vizuri katika mabwawa,mito, madimbwi na mitaro inayotuhamisha maji kwa

muda mrefu kazi yake kubwa hufyonza nitrogen kutoka kwenye hewa pia hukua haraka sana katika maji yaliyotuama.

## FAIDA ZA AZOLLA



1. Hutumika kuongeza nitrogen kwenye udongo kwa kutumika katika utengenezaji wa mbolea vunde au kuyafanya kama matandazo shambani

2. Hutumika kama chakula cha mifugo kwasababu ina kiwango kikubwa cha protein 25%-30% hutumiwa na ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe

3. Huongeza uzalishaji wa maziwa kwa ng'ombe asilimia 15-20

4. Pia hutumika kama tiba ya maji kwani huweza kuyafanya yaweze kutumika kwa muda mrefu inawafaa wale wenye mabwawa ya umwagiliaji

5. Huwasaidia wakulima na wafugaji kupunguza gharama za mbolea na chakula cha mifugo yao

5.Huongeza kipato/faida kwa wafugaji na wakulima

Kilimo cha AZOLLA katika eneo dogo la square mita 18 kina futi 1.5 ambapo unaweza kuvuna AZOLLA ya kula Kuku 100 kila siku.

## MAHITAJI

1. Mbolea ya ng'ombe kilo 27-30
2. Maji
3. Udongo
4. Mbegu ya AZOLLA (culture) kilo 3
5. Mbolea ya kiwandani (single/tripple super phosphate) gram 90-100.

.

Kwa maeneo mengi sana hapa nchini imekuwa changamoto hupatikanaji pamoja na bei za vyakula vya kuku, na watu wengi wamekuwa wakipata wakati mgumu na kufanya ufugaji kuwa na changamoto nyingi na hata kuhahirisha kufanya ufugaji.

Bali sasa vitambue vyakula ambavyo mfugaji unaweza zalisha katika mazingira yake kwa lengo la kulisha kuku wake.

Vifuatavyo ni vyanzo vya chakula ambavyo vyaweza tumika kulisha kuku.

# MMEA WA AZOLA.



Huu ni mmea ambao hukua ndani ya muda mfupi na uweza lisha mfugo wako wa kuku na kuwapatia chanzo kizuri cha protini pamoja na viini lishe vinginevyo.

## MAZINGIRA YA UZALISHAJI

- Eneo ambalo litatumika hakikisha lina funikwa vyema kuweza zuia upotevu mkubwa wa maji, na kuchanganyana na uchafu wa ain ayeyote.

- Eneo lisiwe na shughuli nyingine kuepuka kuchanganyikana na uchafu mwingine pamoja na sumu zingine.



# JINSI YA KUOTESHA



Andaa bwawa square mita 18 kina futi 1.5 au chombo chochote chenye ukubwa wowote unao endana na ukubwa wa eneo ulilo nalo.

Kisha weka nailoni ngumu au turubahi ambalo lituzuia kupotea kwa maji Kunywea chinina Baada ya hapo weka samadi udongo kilo 27-30 mbichi ya ng`ombe ambayo itachukua eneo la inchi 10, ondoa uchafu wote hutakao jitokeza baada ya kuweka samadi juu ya maji hayo.

kisha weka mbegu kiasi cha kilo tatu (3), katika bwawa hilo maalumu.

Baada ya azola kuota Subiri kuvuna baada ya siku 15 kwa Mara ya kwanza baada ya hapo utakuwa ukivuna kila baada ya siku 2-3 kwa zaidi ya mwaka anza kuvuna na kuwapatia kuku wako, baada ya hapo anza kulisha kulingana na wingi wa mifugo ulio nao.

## NAMNA YA KUWALISHA.



Kuna namna mbili kuu za kuwalisha kuku,

Namna ya kwanza kwa kuwapatia kwa kuchanganya na vyakula vingine kwa kuweka azolla kilo 50, pumba kilo 25, na kilo 25 za chakula cha madukani/ ulichochanganya mwenyewe ili kupata kilo 100

Namna ya pili kwa kuwapatia Chakula cha Azolla tu bila chakula kingine.....................................................
..........................................................................

.....................**MWISHO**........................

## KWA MAHITAJI YA YA HUDUMA ZIFUATAZO

- ✓ Vifaranga siku,wiki na mwezi aina zote
- ✓ Mayai ya kuku ya kutotoleasha aina ya SASSO na KROILER
- ✓ Usimamizi wa mradi wa ufugaji kuku
- ✓ Ushauri Zaidi juu ya ufugaji
- ✓ Uandishi wa mchanganuo biashara ya ufugaji ✓ Utafutaji wa masoko ya ufugaji.
- ✓ Vifaranga vya bata vya siku moja
- ✓ Mayai ya bata kwa ajili ya kutotolesha

# WASILIANA NAMI KWA MAWASILIANO

NAMBA ZA SIMU: 06564469991 Tigo

0620765518 Halotel

BARUA PEPE : Godwinmbwambo111